

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

YAFUNDA WATUMISHI 193

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

1.0 UTANGULIZI.

Ndg msomaji Ijumaa ya wiki iliyopita tulipata fursa ya kuangalia malalamiko yaliyoshughulikiwa na Tume katika kipindi cha 2004/2005, 2005/2006 na 2006/2007 ambapo katika kipindi hicho jumla ya malalamiko 29774 yalishughulikiwa. Katika makala ya leo tutapata fursa ya kuangalia jinsi Tume ilivyowaendeleza watumishi wake ili kujenga uwezo wa utekelezaji wa majukumu yake. Ndg msomaji sote tunaelewa kuwa elimu ina thamani kubwa sana katika Taasisi au Jamii yo yote ile duniani. Bila elimu au elimu duni haiwezi kuleta ufanisi au tija katika sehemu yo yote ile ya kazi, hivyo ili Taasisi iweze kufanya kazi na kupata matokeo mazuri, haina budi kuajiri watumishi wenye sifa zinazohitajika na kuwaendeleza watumishi hao ili waweze kumudu mabadiliko mbali mbali ya kiteknolojia, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Sera ya Menejimenti na Ajira ya mwaka 1999 ambayo ndiyo chimbuko la Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 imetoa maelekezo ya namna ambavyo watumishi wa Umma wanaweza kuendelezwa na waajiri wao ili kuzijengea Taasisi za Serikali uwezo wa kiutendaji katika huduma zitolewazo na Serikali kupitia utumishi unaozingatia sifa na usimamizi unaopima matokeo ya kazi. Kwa kuzingatia hili Tume ya Utumishi wa Umma imeandaa mpango wa mafunzo na kutenga bajeti kila mwaka

kwa ajili ya kuwaendeleza watumishi ili wawe na uwezo na ubora katika masuala ya Uongozi, mbinu za Utawala, stadi za kiufundi pamoja na moyo wa kufanya kazi kwa ushirikiano. Katika utekelezaji wa mpango huo Tume imewaendeleza watumishi wake **193** katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Miongoni mwa mafunzo yaliyotolewa na Tume kwa watumishi wake ni pamoja na mafunzo ya ukaguzi, ambapo kwa sasa Tume inafanya ukaguzi kwa kuwatumia watumishi wake wenyewe.

2.0 IDADI YA WATUMISHI WALIOENDELEZWA.

Tume imewaendeleza watumishi **193** katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Idadi ya watumishi waliopolekwa ktika mafunzo ya muda mrefu ni **133** kutoka katika Idara mbali mbali za Tume ambazo ni Idara ya Utawala, Idara ya Afya, Idara Utumishi Serikali, Idara ya Utumishi wa Walimu, Idara ya Utumishi ya Serikali za Mitaa na Idara ya Utumishi ya Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji.

3.0 IDADI YA WADAU WALIOPATA MAFUNZO.

Pamoja na juhudi za Tume za kuwaendeleza watumishi wake kielimu na ujuzi, Tume pia imekuwa ikiwaelimisha wadau wake katika warsha na mikutano mbalimbali ili kuimarisha zaidi uwezo wa Tume wa kutekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwaka 2004/2005, 2005/2006 na kipindi cha mwaka 2006/2007. Katika kipindi hicho jumla ya wadau 1885 walielimishwa na Tume kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Kanuni na Taratibu zake,

miongozo na nyaraka mbalimbali zinazohusu masuala ya ajira na nidhamu. Juhudi za kufanya mafunzo hayo, zimeongeza uelewa na uwezo kwa wadau katika utekelezaji wa masuala ya ajira na nidhamu ambapo Mamlaka zimeweza kuajiri na kuchukua hatua za kinidhamu kwa kuzingtia Sheria, Kanuni na Taratibu zake.

4.0 HITIMISHO.

Siri ya ufanisi wa utendaji wa chombo cho chote cha Serikali [Tume ya Utumishi wa Umma ikiwemo] ni uwezo na ubora wa watumishi wake katika masuala ya uongozi, mbinu za Utawala, stadi zao za kiufundi pamoja na moyo wa kufanya kazi kwa ushirikiano. Kwa hiyo ni muhimu kuhakikisha kwamba kila mtumishi wa sekta yo yote Serikalini anapata ujuzi na sifa zinazofaa na kwamba anajiendeleza daima kimaarifa ili kuboresha utendaji wake. Aidha, wadau wa Taasisi husika ya Serikali nao pia wanahitaji kupata taarifa muhimu na elimu ili Taasisi inapotekeleza majukumu yake isipate shida ya utekelezaji wa majukumu yake na hivyo kuboresha huduma zake.

Ndugu, Msomaji iwapo una maswali, maoni au ushauri tafadhali wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo:

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

Simu: 022 – 2126811 – 4.

